**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu,**

**Mkuu wa Shule 0768 056 996**

**Makamu Mkuu wa Shule 0756553999**

**Malezi 0762 186 070**

**Shule ya Sekondari JJ. MUNGAI**

**S.L.P. 226 MAFINGA**

**2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JJ. MUNGAI HALMASHAURI YA MJI MAFINGA MKOA IRINGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari JJ MUNGAI ipo umbali wa Kilometa 3.1 Magharibi mwa Mji wa MAFINGA. Usafiri wa bajaji ni shilingi 3000, kwa pikipiki shilingi 2000 na Shilingi 5,000 kwa gari (taxi).

Muhula wa Masomo utaanza kadri utakapotangazwa na waziri Elimu kwenye vyombo vya habari.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1: Sare za Shule (WASICHANA)**

1. Sketi za rangi ya maroon mbili (siyo damu ya mzee) zenye marinda box na zilizo ndefu kufika chini, makoti mawili (ya kitambaa cha sketi) pamoja na tai.(suti)
2. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni la blue (Esteem Material).
3. Jezi ya pink iliyoandikwa jina la mwanafunzi kwa nyuma.
4. Rangi ya hijabu kwa waislam tu (kijuba) iwe nyeupe na isiyo na urembo, rangi nyingine haziruhusiwi.
5. Mashati meupe mikono mirefu mawili.
6. Soksi nyeupe jozi mbili
7. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi.
8. Tracksut ya rangi bluu nzito **isiyo ng'aa** wala isiwe na **kofia**.
9. Pull neck nyeusi
10. Jaketi jeusi liliso na maandishi wala kofia **(Maprova na majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi shuleni)**

11. Aje na raba nyeupe kwa ajili ya michezo jozi moja ambazo atazivaa muda wa michezo tu. Michezo kwetu ni taaluma hivyo ni lazima.

**(B) WAVULANA.**

1.Suruali mbili (2), makoti mawili rangi ya maroon, pamoja na tai.(suti)
2.Nguo ya kushindia (shamba dress) yaani suruali ya blue ambayo itavaliwa na tshirt ya bluu (Esteem Material).
3.Jezi ya pink iliyoandikwa jina la mwanafunzi kwa nyuma.
4.Mashati meupe mikono mirefu mawili.
5.Soksi nyeupe jozi mbili.
6.Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
7.Traksut ya rangi ya bluu nzito **isiyo ng'aa** wala isiwe na **kofia**.
8.Pull neck nyeusi
9.Jaketi jeusi liliso na maandishi wala kofia (Maprova na majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi shuleni).
10. Aje na viatu vya michezo jozi moja ambavyo atavivaa muda wa michezo tu. Michezo kwetu ni taaluma hivyo ni lazima

**MUHIMU: SARE ZOTE ZITASHONWA SHULENI KUEPUKA KUCHANGANYA RANGI ZINGATIA:**

- ✓ Mavazi mengine tofauti na yale yaliyoelekezwa hayaruhusiwi kabisa, ukaguzi utafanyika ili kuhakiki vifaa alivyokujanavyo mwanafunzi shuleni.
- ✓ Nguo zote za shule zitawekewa muhuri wa shule kwa gharama ya mzazi shilingi 2000 kwa kila nguo.

**2.2: Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i Ream ya karatasi (**A4**) 2 kwa mwaka

ii File 3 (spring file) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi

iii Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

iv Scientific calculator

v Godoro kwa wanafunzi (futi 2 ½) Dodoma TX cover

vi Blanket 1 la kawaida kwani mazingira ni ya baridi

vii Mashuka 2, 1 rangi ya pink na 1 rangi ya light blue

vii**i** Tranka imara kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyake

ix Vifaa vya chakula na vyombo vingine: kontena, kikombe cha chai, kikombe cha kuogea, kijiko 1 na ndoo za plastiki 2. Vinapatikana jirani na eneo la shule.

x. Kanda mbili za bata au umoja, na gambuti rangi nyeusi tu (Zinapatikana maeneo ya karibu na shule).

**KWA UPANDE WA MASOMO MWANAFUNZI AJE NA**

i Daftari kubwa (counter book quire 4) zisizopungua 10

ii Daftari ndogo (msomi) zisizopungua 10

iii Kalamu za kutosha

iv Mkebe (mathematical set)

v School bag ni lazima kwa ajili ya kubebea vifaa vya darasani

**VIFAA VYA USAFI NA MAZINGIRA**

Kila mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi shuleni;

- ✓ Wasichana , **Jembe, Slesha, Squzer na Reki**
- ✓ Wavulana, **Jembe, Slesha, Squzer na Panga**

**1.1 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **75,000/=** |

B. Michango yote iwekwe kwenye **Akaunti Namba 60201200062 NMB Plc** yenye Jina J.J. Mungai Secondary School.

**ZINGATIA KUWA:**
Mwanafunzi anatakiwa aje na kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu yake. Iwapo hana kadi ya bima,atachangia shilingi elfu kumi (10000) ili apate bima ya afya iliyoboreshwa (CHF).

**Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

- **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote shuleni na vifaa mbali mbali vya urembo kama vile perfume, wanja lipstick n.k**

- **Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi unaruhusiwa kuja kumtembelea mwanao kwa siku iliyopangwa na uongozi wa shule ambayo ni mara moja kwa mwezi (kila jumapili ya mwisho wa mwezi). Tafadhari mzazi/mlezi usije na vyakula vya aina yoyote.**

**MPANGO WA USAFIRI.**

- **Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli. Usafiri wa kufika Mafinga ni kwa njia ya mabasi. Mwalimu wa usafiri atakusadia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda na kurudi likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni. Pia kwa mwanafunzi atakayekuwa anatokea mazingira karibu na shule ilipo bhasi tunakuomba mzazi/mlezi uje kumchukua shule zinapofungwa na haturuhusu boda boda kuja kumchukua mwanafunzi kwa ajili ya ulinzi na usalama wa mtoto.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**


i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix. Kuchelewa kuripoti shuleni wakati wa likizo.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v**.** Passport nne (04) za mwanafunzi akiwa amevalia shati jeupe
vi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa**.**
vii. Aje na result slip original ya kidato cha nne.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule: NASHON B. NDANZI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:** 


**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- ➢ **Mkuu wa shule: 0768056996**
- ➢ **Makamu Mkuu wa Shule: 0756553999**
- ➢ **Mwandamizi Malezi: 0762186070**

**USAJIRI WA NECTA: S.0449**

**SEHEMU;D, Fomu Na2 -B**

## TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano wakati wote awapo shuleni. **Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu**.

Jina la mwanafunzi ……………………………………
Kidato…………..mchepuo.................... Mwaka…………

Anwani ya nyumbani (anayotumia)………………………………Tarehe ya kuzaliwa…….……………

Kama ni mlemavu, aina ya ulemavu…………………………………taarifa za wazazi, mzazi moja……………… wazazi wawili………………..yatima ……………..

Namba ya simu(ya nyumbani/ya mzazi)……………………Mtaa/Kijiji anachotoka…………………...Kata…………….
Tarafa………………...Wilaya………………Mkoa…………………..shule ya msingi aliyosoma……………….

Shule ya Sekondari atokayo……………………… Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne……………

Anwani ya shule ……………………….Matokeo yake ya kidato cha nne………………………………

Dini yakeni …………………[Mkristo, Mwislamu n.k.]Dhehebu lakeni……………… Mkatoliki, Mlutheri,Suni n.k}

Sahihi ………………………………… Tarehe……………………………...

**NB. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili Dini akiwa shuleni.**

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi……………………………………….. NAKUBALI / SIKUBALI nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari J.J.MUNGAI. Naahidi kuwa nitazitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote nitakaokaa J.J.MUNGAI Sekondari. Nakiri kuwa kwa akili zangu timamu, taarifa zote nilizotoa hapo juu ni sahihi na zinanihusu.

Jina ……………………………………….. sahihi ………………………Tarehe ………………..…

## TAARIFA YA MZAZI/ MLEZI

Jina la Mzazi/ Mlezi ……………………………………………………………………….

Anwani yake………………………………………………………………………………

Namba ya simu ……………………………………………………………………………..

Kazi anayofanya………………………………………………………………………….

Wilaya/Mji anakofanyia kazi………………………………………………………………

Anwani ya kazini…………………………………………………………………………..

Namba ya simu ya kazini
…………………………………………………………………………..............

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi………………………………………..MZAZI/MLEZI NAKUBALI / SIKUBALI nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari JJ MUNGAI. Naahidi kuwa nitawajibika/sitawajibikana kumhimiza mwanangu kuzitii taratibu, kanuni na sheria zote za shule. Nitashiriki/sitashiriki kumhimiza kufuata masharti yote yanayotolewa na Mkuu wa shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa shule. Ninaahidi pia nitashirikiana/sitashirikiana na uongozi wa shule kumhimiza mwanangu kushirikiana na wanafunzi wenzake katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo na kuwa na nidhamu kwa muda wote atakaokaa J.J.MUNGAI Sekondari. Nitapenda/sitapenda kupata taarifa zote zinazomhusu mwanangu muda wote awapo shuleni***(futa isiyohusika)***

**Jinalamzazi/mlezi……………………………..Sahihi………………Tarehe…………………**

**WATU WA KARIBU(KIUHUSIANO/UNDUGU)NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/ WALEZI**

(i) Jina………………………………………………… Anwani ……………………………………

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ………………….……………….

Uhusiano wake na mwanafunzi………………………………..........................................................

(ii) Jina **…………………………………………………** Anwani …………………………………….

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ……………….……..…………….

Uhusiano wake na mwanafunzi………………………………..........................................................

(iii) Jina **…………………………………………………….**Anwani ……………………………………

Namba ya simu……………………………… Kazi anayofanya ………………….……………….

Uhusiano wake na mwanafunzi………………………………......................................................

***NB; Iwapo anwani ya mmojawapo wa Mzazi/Mlezi au ndugu wa karibu amehama au Amefariki lazima mwanafunzi atoe taarifa na kubadilisha jina na kuandika mtu mwingine ambaye atawajibika kwa mwanafunzi***

**SEHEM; E, Fomu Na 3- C**

**FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya) ………………………………………………..

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)………………………………..

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

**(A) Hali ya Mwili.**

(i) Mapigo ya moyo………………………………………………………
(ii) Damu (Haemoglobin)……………………………………………..…..
(iii) Kundi la Damu (Blood group)……………………….………………...
(iv) Mkojo…………………………………………………………………….
(v) Haja kubwa……………………………………………………………….
(vi) Macho …………………………………………………………………….
(vii) Masikio ………….……………………………………………………..

**NB.** Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa…………………………………..

**Magonjwa.**

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;

(a) Kifua kikuu (TB)……………………………………………………….…
(b) Kifafa (Epilepsy)…………………………………………………………
(c) Shinikizo la damu (BP)…………………………………………………..
(d) Magonjwa ya tumbo ……………………………………………………..
(e) Seli mundu (Sickle cells)…………………………………………….……
(f) Ukoma……………………………………………………………………
(g) Magonjwa ya zinaa (taja aina)……………………………………………
(h) Ugonjwa wa akili ………………………………………………………..…
(i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu ….…………………………..

**Maoni ya Daktari**

…………………………………….……………………………………………

Saini na Muhuri wa Daktari/Mganga wa Hospitali ya Serikali.

**SEHEMU;F,Fomu na4- D**